

Kuna watatu wenyе mwendo wa kupendeza Naam, wanne walio na mwendo mzuri.

SWALI: Naomba kufahamu ni hekima gani tunaipata nyuma ya vifungu hivi, vinavyosema “Kuna watatu wenyе mwendo wa kupendeza, Naam, wanne walio na mwendo mzuri”.

JIBU: Mithali 30:29 “Kuna watatu wenyе mwendo wa kupendeza, Naam, wanne walio na mwendo mzuri. 30 Simba aliye hodari kupita wanyama wote; Wala hajiepushi na aliye yote; 31 Jimbi aendaye tambo; na beberu; Na mfalme ambaye haasiki”.

Swali la kujiuliza ni kwanini wameonekana wana mwendo mzuri na wa kupendeza, jibu ni kwasababu ya tabia yao ya ujasiri na kuamini kuwa wao ni wamiliki.

kwamfano **Simba** ni mfalme wa pori, kila kitu kilicho mbele yake anakiona ni chakula, hivyo hana uoga na lolote. Anamiliki wanyama wote , hata wale wanaoonekana ni wakubwa na wenyе nguvu kuliko yeye. Wote wanamkimbia.

Anamtaja pia **jimbi/jogoo**, ambaye na yeye ni mfalme wa shamba, usemi wa “kutanua mbawa” umeanzia kwake. Yeye anaamini anaweza kumiliki mitetea yote na kundi lote la kuku. Watafiti wanasema kule

Kuna watatu wenyewe mwendo wa kupendeza Naam, wanne walio na
mwendo mzuri.

kuwika kwa jogoo, sio bila sababu tu. Hapana, bali ni anatuma ujumbe
kwa majogoo wengine wasimsogelee kwenye miliki yake na kutafiti
kama yupo ambaye anamkaribia, ajiandae kwa mapambano. Tofauti na
ndege wengine walio madume, hawana tabia za kujimilikisha kama
Jogoo, au kupigana ili kumiliki shamba.

Anamtaja pia **Beberu**,(Mfalme wa zizi) katika kundi, beberu
utamtambua tu kwa tabia zake, hujiaminisha sana, muda wote hatulii,
analimiliki kundi lote kana kwamba yeeye ndio mchungaji-msaidizi
(Zekaria 10:3). Katika Historia unabii wa Aleksanda mkuu aliyetawala
Ugiriki ya kale, ambaye aliteka ngome nyingi sana, kila alipopatamani
alikwenda na akashinda alifananishwa na beberu katika maandiko
Kutokana na Tabia zake hizo (Danieli 8:5). Hata sasa mataifa
yanayotaka kumiliki mataifa mengine kwasababu ya nguvu zao za
kijeshi, au kiuchumi au kisiasi, hujulikana kama mataifa ya kibeberu.

hiyo ni kufuatana na Tabia ya beberu ya kupenda kumiliki zizi.

Lakini wa mwisho anamtaja pia, **Mfalme asiyreasika**. Ambaye ni
mtawala wa Nchi. Kama tunavyojua wafalme ndio viongozi wa taifa,
humiliki vyote, na yoyote atakayekatiza mbele yake kujaribu
kuuangusha ufalme wake, humuua. Mfalme ni zaidi ya raisi, Wafalme
wengi waliteka ngome kwa vita, sio kwa kuchaguliwa, Ujasiri na

Kuna watatu wenyewe mwendo wa kupendeza Naam, wanne walio na mwendo mzuri.

misimamo yao huwamilikisha.

Ni hekima gani tunaipata?

Hivyo mwandishi wa mithali anajaribu kuonyesha , ujasiri na ushujaa ambao na sisi tunaweza kuupata endapo tutakuwa ndani ya Kristo. Bwana atatufanya tuwe na roho kama za wanyama hawa, mienendo yetu itakuwa bila WOGA sikuzote. Tutaishi kama watu wasio na mashaka kwa lolote. Hatutaogopa wanadamu, wala matatizo, wala wachawi, wala magonjwa, wala shida yoyote. Kwasababu tunajua uwezo wa kuyashinda hayo na kuyamiliki tunao mfano wa Simba na mfalme.

Bwana Yesu aliye mfalme wetu, anayemiliki sasa mbinguni na duniani, Simba wa Yuda, aliyashinda na sisi pia tutayashinda endapo tutakuwa ndani yake alisema hivyo.

Yohana 16:33 "...jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu".

Je! Utapenda kumpa leo Yesu maisha yako? Ili aanze upya na wewe,akupe tumaini jipyla uzima wa milele? Na ujasiri wa kuishi hapa duniani bila woga?

Kuna watatu wenyе mwendo wa kupendeza Naam, wanne walio na
mwendo mzuri.

Kama jibu ni ndio basi fuatiliza mwongozo huu, na Leo Leo utaupokea
wokovu >> **KUONGOZWA SALA YA TOBA**

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

**Jiunge na kundi letu la mafundisho ya Biblia whatsapp kwa
kubofya hapa >> **WHATSAPP-GROUP****

Mada Nyinginezo:

MWENDO UNAOSHANGAZA SANA!

**NI NINI KITAKACHOTUFANYA TUPIGE MBIO BILA KUPUNGUZA
MWENDO?**

Biblia inamaana gani kusema “vipo sita, naam saba”?

Ni kwa namna gani Yesu ni Simba wa Yuda?

Kuna watatu wenyewe mwendo wa kupendeza Naam, wanne walio na
mwendo mzuri.

**Je ni kweli Isaka alifarijika kwa kifo cha mamaye? (Mwanzo
24:67)**

Kupwelewa maana yake nini? (Matendo 27:26).

YATAMBUE MAJIRA YA KUJILIWA KWAKO.

INAYOENDELEA SASA NI HUDUMA YA RUTHU.

Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp